**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE**

Tarehe: **23/08/2023**

## TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI (MKATABA MWAKA 1).

Ofisi ya Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke inawatangazia nafasi za kazi( mkataba kwa mwaka mmoja) katika Hospitali na vituo vya Afya vifuatavyo:- **Hospitali ya Mbagala Rangi tatu, Zahanati ya Sigara, Zahanati ya Sandali, Kituo cha afya Kijichi, Zahanati ya Kizuiani, Kituo cha Afya RoundTable, Kituo cha Afya Majimatitu, Zahanati ya Charambe, Zahanati ya Kilakala, Zahanati ya Kichemchem, Zahanati ya Chang'ombe, Zahanati ya Kigugi, Kituo cha Afya Buza, Kituo cha Afya Yombo Vituka, Zahanati ya Tandika, Zahanati ya Mikwambe, Zahanati ya Makangarawe, Zahanati ya Tambukareli, Zahanati ya Miburani, Zahanati ya Mzinga, Zahanati ya Toangoma, Zahanati ya Chamazi, Zahanati ya Mtoni na Zahanati ya Mbande** Hivyo Watanzania wote wenye sifa na uwezo wa kujaza nafasi tajwa hapo chini watume maombi.

### 1. DAKTARI DARAJA LA II- (NAFASI 2)

**(A)SIFA ZA KUAJIRI**

(i) Awe amehitimu kidato cha sita na kufaulu

(ii) Awe amehitimu Shahada ya Udaktari kutoka Vyuo Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza "Internship" na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika)

**(B) KAZI NA MAJUKUMU**

(i) Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura.

(ii) Kutoa na kusimamia elimu ya afya pamoja na kuboresha afya ya jamii katika Wilaya na Mikoa au eneo lake la kazi.

Scanned with CamScanner

Scanned with CamScanner

(iii) Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa Kutunza takwimu na kuzitumia kama inavyoelekezwa katika misingi ya MTUHA.

(iv) Kufundisha wanafunzi na watumishi waliopo kwenye eneo la kazi

(v) Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement)

(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**2. TABIBU DARAJA LA II – (NAFASI 9)**

**A) SIFA ZA KUINGILIA MOJA KWA MOJA:**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne/sita wenye Stashahada ya Tabibu/Tabibu Meno kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali.

***B) KAZI NA MAJUKUMU:***

(i) Kazi zote zinazofanywa na Tabibu Msaidizi

(ii) Kutambua na kutibu magonjwa ya kawaida

(iii) Kusimamia utendaji wa watumishi walio chini yake na kufanya upasuaji mdogo.

(iv) Kushiriki katika kupanga na kutekeleza Huduma za Afya Msingi

(v) Kushauri na kuhamasisha wananchi kuchangia huduma za Afya za Mfuko wa Afya ya Jamii

(vi) Kuweka kumbukumbu za vifaa na zana za kutolea huduma

(vii) Kuweka kumbukumbu, kuandaa na kutoa taarifa za utekelezaji

(viii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

**3. MTEKNOLOJIA DARAJA II – RADIOGRAFA (MIONZI/RADIOLOJIA) (NAFASI 4)**

**(A) SIFA ZA KUAJIRIWA;**

Kuajiriwa wenye Stashahada (Diploma) katika fani ya Uteknolojia katika fani ya radiolojia kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU:**

(i) Kuwapima wagonjwa wanaoelekezwa kwenye eneo lake la kazi

(ii) Kutunza mitambo na vifaa vya Radiolojia katika eneo lake la kazi

Scanned with CamScanner

(iii) Kukagua picha za X-Ray zilizopimwa kwa ubora na kutosheleza (diagnostic quality)

(iv) Kutunza picha za wagonjwa hadi majibu yanapowafikia madaktari waliowatuma wagonjwa.

(v) Kutoa Ushauri kuhusu masuala ya na kazi za Radiolojia na Mionzi katika eneo lake la kazi.

(vi) Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization).

(vii) Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi.

(viii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**4. MTEKNOLOJIA DARAJA II – RADIOGRAFA – ULTRA SOUND (NAFASI 6)**

***(A)* SIFA ZA KUINGILIA MOJA KWA MOJA:**

Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia katika ya fani ya Radiotherapia kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

**(B)KAZI NA MAJUKUMU:**

(i) Kutibu wagonjwa wanaolekezwa kwenye eneo lake la kazi kwa mionzi sahihi iliyoelekezwa na Dakitari Bingwa wa Mionzi

(ii) Kutunza mitambo na vifaa vya Radiotherapia katika eneo lake la kazi

(iii) Kukagua na Kusimamia ubora wa mionzi inayotolewa na mitambo ya Radioterapia (Radio-therapeutic quality)

(iv) Kusimamia watumishi walio chini yake

(v) Kutoa Ushauri kuhusu masuala ya kazi za Radiotherapia na Mionzi katika eneo lake la kazi.

(vi) Kuandaa vifaa vya tiba/uchunguzi na kusimamia utakasaji vifaa katika eneo lake la kazi (sterilization)

(vii) Kutoa mafunzo ya awali kwa watumishi wanaopangiwa kazi katika eneo lake la kazi

(viii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

Scanned with CamScanner

**(A) SIFA ZA KUINGILIA MOJA KWA MOJA:**

Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia katika fani ya Maabara kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

**(B)KAZI NA MAJUKUMU:**

(i) Kupima sampuli zinazoletwa maabara.

(ii) Kuhifadhi sampuli zinazotakiwa kufanyiwa uchunguzi au kupelekwa Maabara za ngazi za juu.

(iii) Kufanya kazi za ukaguzi wa maabara, vitendanishi, vifaa, kemikali na hifadhi ya kemikali

(iv) Kuweka kumbukumbu za maabara ambazo zimepatikana wakati wa uchunguzi.

(v) Kufundisha watumishi walio chini yake.

(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake.

**6. MTEKNOLOJIA DARAJA II – DAWA – (NAFASI 11)**

**(A) SIFA ZA KUINGILIA MOJA KWA MOJA:**

Kuajiriwa wenye Stashahada katika fani ya Uteknolojia katika ya fani ya Madawa kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza pale inapohusika.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU:**

(i) Kuainisha, kuandaa na kuagiza mahitaji ya dawa na vifaa tiba katika eneo lake la kazi.

(ii) Kugawa dawa na vifaa tiba kwa wagonjwa na watumishi

(iii) Kuhifadhi dawa na vifaa tiba

(iv) Kuelimisha jamii kuhusu matumizi sahihi ya dawa

(v) Kukagua dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi katika eneo lake la kazi

(vi) Kutoa taarifa juu ya madhara yatokanayo na matumizi ya dawa.

(vii) Kuandaa taarifa ya matumizi ya dawa na vifaa tiba

Scanned with CamScanner

(viii) Kufanya kaguzi mbalimbali katika sehemu zinazohifadhi dawa.

(ix) Kutunza kumbukumbu za dawa na vifaa tiba

(ix) Kuchanganya dawa

(x) Kuratibu kazi za kamati ya dawa ya hospitali

(xi) Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi

(xii) Kufanya uchunguzi wa ubora wa dawa, vifaa tiba kemikali, vitendanishi na vipodozi

(xiii) Kusimamia utendaji wa kazi watumishi walio chnini yake

(xiv) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

## 7. MTEKNOLOJIA MSAIDIZI –DAWA (NAFASI 4)

### A. SIFA ZA KUINGIALIA MOJA KWA MOJA:

Kuajiriwa wenye cheti katika fani zilizotajwa hapo juu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza yao pale inapohusika.

### B. KAZI NA MAJUKUMU:

(i) Kuandaa vitendanishi (reagents) vya kufanyia vipimo vya Maabara.

(ii) Kufanya kazi za awali sampuli zinazoletwa maabara

(iii) Kukusanya damu kutoka kwa wagonjwa na watu wanaojitolea

(iv) Kurekodi matokeo ya vipimo kwenye regista

(v) Kutayarisha vifaa vya kazi.

(vi) Kuhifadhi kwa mujibu wa taratibu sampuli zote zinazohitaji kuhifadhiwa baada ya uchunguzi.

(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wakeujuzi wake zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

Scanned with CamScanner

**7. MTEKNOLOJIA MSAIDIZI –MAABARA (NAFASI 1)**

**(A) SIFA ZA KUINGIALIA MOJA KWA MOJA:**

Kuajiriwa wenye cheti katika fani zilizotajwa hapo juu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali na ambao wamesajiliwa na Mabaraza yao pale inapohusika.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU**

(i) Kuandaa vitendanishi (reagents) vya kufanyia vipimo vya Maabara.
(ii) Kufanya kazi za awali sampuli zinazoletwa maabara
(iii) Kukusanya damu kutoka kwa wagonjwa na watu wanaojitolea
(iv) Kurekodi matokeo ya vipimo kwenye regista.
(v) Kutayarisha vifaa vya kazi.
(vi) Kuhifadhi kwa mujibu wa taratibu sampuli zote zinazohitaji kuhifadhiwa baada ya uchunguzi.
(vii) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

**8. USTAWI WA JAMII DARAJA LA II – (NAFASI 1)**

**(A) SIFA ZA KUINGILIA MOJA KWA MOJA**

Kuajiriwa wenye Shahada ya B.A (Social Work or Sociology) au Stashahada ya juu ya Ustawi wa Jamii (Advanced Diploma in Social Work) kutoka Chuo cha elimu ya Juu kinachotambuliwa na Serikali.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU**

*(i)* Kuendesha usaili kwa wahudumiwa (watu wenye ulemavu, wazee, familia zenye matatizo, watoto na washitakiwa).

*(ii)* Kufanya ukaguzi wa mazingira wanayoishi wahudumiwa ili kupata taarifa zao kamili.

Scanned with CamScanner

*(iii)* Kupokea na kukusanya takwimu zinazohusu huduma za watu wenye ulemavu wazee, malezi ya watoto na familia zenye matatizo.

*(iv)* Kupokea, kuchambua na kuandaa orodha ya maombi mbalimbali kutoka kwenye familia na watu wenye dhiki.

*(v)* Kuhoji na kuanda taarifa za washtakiwa

*(vi)* Kusimamia wahudumiwa katika makazi, vyuo vya mafunzo ya Ufundi Stadi vya watu wenye ulemavu, Mahabusi za Watoto na Shule ya Maadilisho.

(xv) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

### *9. AFISA MUUGUZI MSAIDIZI DARAJA LA II – (NAFASI 9)*

**A. SIFA ZA KUAJIRIWA MOJA KWA MOJA**

Kuajiriwa wenye Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

**B. KAZI NA MAJUKUMU:**

(i) Kutoa huduma za uuguzi

(ii) Kukusanya takwimu muhimu za afya.

(iii) uwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake

(iv) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya

(v) Kutoa huduma za kinga na uzazi

(vi) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake

### 10. MUUGUZI DARAJA LA II – (NAFASI 28)

***(A)* SIFA ZA KUAJIRIWA MOJA KWA MOJA**

Kuajiriwa wenye cheti cha Uuguzi cha miaka miwili kutoka katika Chuo kinachotambuliwa na Serikali na kuandikishwa (Enrolled) na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania.

**(B) KAZI NA MAJUKUMU**

**(i)** Kufanya kazi kiuguzi za kuhudumia wateja katika jamii, hospitali na sehemu zote zinapotolewa huduma za afya

(ii) Kusimamia kuratibu kazi zote za wahudumu wa afya katika sehemu yake ya kazi
(iii) Kukusanya takwimu na kutayarisha taarifa za utendaji wake wa kazi .
(iv) Kutoa ushauri nasaha
(v) Kutoa huduma za kinga na uzazi wa mpango
(vi) Kutoa huduma za uzazi na afya ya mtoto
(vii) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya
(viii) Kufuatilia utunzaji wa vitendea kazi katika maeneo yake ya kazi
(ix) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu uzoefu na ujuzi wake

## 11. AFISA HESABU DARAJA LA II(ACCOUNTS OFFICER II) (NAFASI 3)

### A. SIFA ZA KUJIUNGA MOJA KWA MOJA

Kuajiriwa wenye Intermediate certificate(Module D) inayotolewa na NBAA au sifa nyingine zinazolingana na hizo zinayotambulika na NBAA, shahada ya Biashara/Sanaa aliyejiimarisha kwenye fani ya Uhasibu au shahada ya Juu ya uhasibu kutoka Taasisi yoyote inayotambuliwa na serikali.

### B. KAZI NA MAJUKUMU YA KUFANYA

(i) Kushiriki kuandika taarifa ya mapato na matumizi
(ii) Kushiriki mhasibu kuandaa taarifa za maduhuli
(iii) Kushiriki kufanya usuluhisho wa hesabu za benki na nyingine zinazohusiana na masuala ya fedha
(iv) Kuandaa taarifa mbalimbali za mishahara
(v) Kuandika hati za malipo na hati za mapokezi.
(vi) Kutunza daftari la amana
(vii) Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi

Scanned with CamScanner

. 13. *MSAIDIZI WA AFYA- HEALTH ATTENDANT (NAFASI 11)*

**A) SIFA ZA KUJIUNGA MOJA KWA MOJA**

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne wenye cheti cha mafunzo ya Msaidizi wa Afya au Fundi Sanifu Afya Mazingira kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

**B) KAZI NA MAJUKUMU:**

(i) Kufanya usafi wa vifaa vya kazi, usafi wa wodi na mazingira

(ii) Kusaidia wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza katika kwenda haja (kubwa na ndogo) na kuoga

(iii) Kumsaidia kumlisha mgonjwa asiyejiweza

(iv) Kuchukua nguo za mgonjwa kuzipeleka kwenda kufuliwa

(v) Kuchukua sampuli za mgonjwa kwa ajili ya vipimo vya maabara na kufuatilia majibu

(vi) Kutayarisha vifaa kwa ajili ya kusafisha na kufunga majeraha

(vii) Kufuatilia mahitaji ya dawa kwa wagonjwa kutoka hifadhi ya dawa.

(viii) Kufanya shughuli nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi.

Maombi yatumwe kwa :

**MKURUGENZI ,**

**HALMASHAURI YA MANISPAA YA TEMEKE,**

**S.L.P 46343,**

**DAR ES SALAAM.**

**Mwisho wa kutuma maombi ,siku saba kuanzia tarehe ya Tangazo hili.**

G. B. Mtisho

**Kny.MKURUGENZI WA MANISPAA**

Kny: Mkurugenzi Mtendaji
Manispaa Ya Temeke

Scanned with CamScanner